



**BENKI KUU YA TANZANIA**

**MAJIBU YA MASWALI  
YAUUZWAYO MARA KWA MARA**



**BENKI KUU YA TANZANIA**

**MAJIBU YA MASWALI  
YAUUZWAYO MARA KWA MARA**

**KURUGENZI WA UTAFFITI NA  
SERA ZA UCHUMI**

**TOLEO LA 2019**

**© Kurugenzi wa Tafiti na Sera za Kiuchumi**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi  
Benki Kuu ya Tanzania,  
Mtaa wa 2 Mirambo  
11884, Dar es Salaam.  
Simu: +255 22 2233328/9, +255 22 2233330,  
Nukushi: +255 22 2234060  
Tovuti: <http://www.bot.go.tz>

## **UTANGULIZI**

Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikitoa machapisho mbalimbali yenye lengo la kuelimisha umma kuhusu majukumu na kazi zake, na masuala mbalimbali ya uchumi. Machapisho hayo ni pamoja na ripoti za uchumi za mwezi, robo mwaka na mwaka mzima, na Tamko la Sera ya Fedha.

Mbali na machapisho hayo yanayotoa taarifa mbalimbali, Benki Kuu imekuwa ikipokea maswali mbalimbali yanayohusu masuala ya kiuchumi na utendaji wake. Maswali hayo yamekuwa yakiulizwa na wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi, waandishi wa habari, Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na wananchi kwa ujumla. Maswali hayo yanaulizwa kupitia Bunge na Baraza la Wawakilishi, maonesho ya sabasaba na nane nane, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, na wadau mbalimbali wanaotembelea ofisi za Benki Kuu.

Maswali hayo yanayohusiana na majukumu ya Benki Kuu katika kusimamia uchumi wa nchi kwa ujumla, hususan, sera ya fedha na mfumuko wa bei, usimamizi wa mabenki, utoaji na usimamizi wa sarafu, uhifadhi wa hazina ya fedha za kigeni, huduma za kibenki, thamani ya shilingi, na utangamano wa kiuchumi wa kikanda hususan Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Baadhi ya maswali yamekuwa yakijirudia mara kwa mara, na Benki Kuu imekuwa ikitoa majibu ya maswali hayo kupitia njia mbalimbali. Hivyo, katika muendelezo huo, Kurugenzi ya Tafiti na Sera za

Kiuchumi imechapisha kitabu hiki kwa lengo la kuwezesha wadau mbalimbali kufanya marejeo ya maswali na majibu, na kuongeza uwazi katika sera ya fedha na shughuli za Benki Kuu.

Majibu ya maswali haya, yameandikwa kwa lugha nyepesi ili kuwaelimisha Watanzania wengi pasipo kuhitaji elimu kubwa ya taaluma ya uchumi. Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wote kwa ujumla ambao ndiyo msingi wa maswali haya, na ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakidhi mahitaji ya wadau wa Benki Kuu.

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **MFUMUKO WA BEI NA SERA YA FEDHA**

- 1. Benki Kuu inasema mfumuko wa bei umedhibitiwa wakati bei za vitu muhimu zinapanda kila kukicha. Nini maelezo yake?**

Mfumuko wa bei hupimwa kwa kuangalia fahirisi ya bei kitaifa katika kapu la bidhaa na huduma mbalimbali za jamii kwa kipindi fulani kwa mfano mwaka mmoja au hata mwezi mmoja. Katika kapu hilo linalotumiwa kukokotoa mfumuko wa bei vinaweza kuwemo vitu ambavyo vimepanda bei sana na vingine ambavyo vimepanda kidogo na hata wakati mwingine kushuka. Kwa vile fahirisi inaangalia wastani, tunasema kuwa kwa wastani kasi ya upandaji wa bei imekuwa tulivu sawa na malengo ya sera ya fedha.

leleweke pia kwamba, mfumuko wa bei unaposhuka haimanishi kwamba bei za vitu muhimu zimeshuka bali kasi ya upandaji bei kwa ujumla imepungua ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

**2. Benki Kuu hupunguza ukwasi kama njia ya kudhibiti mfumuko wa bei, kwanini isitumie njia ya kuongeza uzalishaji?**

Benki kuu hutumia njia kuu mbili katika kudhibiti mfumuko wa bei. Njia ya kwanza ni ile ya kudhibiti ujazi wa fedha ili uendane na mahitaji halisi ya kiuchumi. Njia ya pili ni ile ya kuimarisha utulivu wa thamani ya sarafu ya nchi husika dhidi ya sarafu za nchi za kigeni hususan zile ambazo zina mahusiano ya karibu ya kibiashara.

Njia hizi pekee za Benki Kuu hazijitoshelezi kudhibiti mfumuko wa bei kama hatua nyingine sambamba na hizi hazitachukuliwa. Hatua hizi ni pamoja na sera nzuri ya Serikali ya mapato na matumizi, na uzalishaji wa vitu na huduma kwa wingi unaoendana na mahitaji ya kiuchumi.

**3. Je, hatua gani huchukuliwa na Serikali katika kudhibiti mfumuko wa bei kwa mambo yaliyo nje ya uwezo wake kama vile kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia.**

Kupanda kwa bei ya mafuta ni tatizo linaloathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi. Pamoja na kwamba nchi kama Tanzania haina ushawishi katika kuamua mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia, zipo hatua mbalimbali zinazoweza kutekelezwa ili kudhibiti madhara yatokanayo na kupanda kwa bei za mafuta: -

- i. Serikali kupanua wigo wa mapato yake ili kupunguza utegemezi wa kodi inayotokanayo na mafuta kutoka nje, hivyo kupunguza bei ya mafuta.
- ii. Kupunguza utegemezi wa umeme utokanao na mafuta na badala yake kuongeza matumizi ya gesi asilia, umeme wa maji, mkaa ya mawe, upepo n.k.
- iii. Serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kudhibiti ongezeko holela la bei za mafuta kwa kuhakikisha kuwa bei za mafuta zinaendana na hali halisi ya upatikanaji wa nishati hiyo nchini.
- iii. Serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuendelea na utaratibu wa manunuzi ya jumla ya mafuta ili kuongeza ushindani ambao utapelekea unafuu wa bei.

#### **4. Uuzaji wa dhamana na hati fungani za serikali unaisaidiaje Serikali katika kudhibiti ujazi wa fedha?**

Dhamana na Hati Fungani za Serikali huuzwa kwa mnada na Benki Kuu kwa niaba ya Serikali na kununuliwa na umma zikiwemo taasisi za kifedha, watu binafsi na mashirika mbalimbali.

Dhamana za serikali ndio zinazotumika kudhibiti ujazi wa fedha. Wanunuzi wa dhamana hizi huzilipia kwa fedha taslimu



zinazopokelewa na kuhifadhiwa na Benki Kuu kwenye akaunti maalum, na hivyo kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi.

**5. Je ni nini kinasabasha viwango vya riba ya dhamana za serikali kushuka?**

Viwango vya riba ya dhamana za serikali kama ilivyo kwa bidhaa yeyote ile kunategemea nguvu za soko. Kushuka kwa riba ya dhamana za Serikali ni kishiria kuwa mahitaji ni makubwa kuliko ugavi. Kuna sababu mbalimbali zinazosababisha mahitaji ya dhamana za serikali kuzidi ugavi zikiwepo;

- i. Kuongezeka kwa idadi ya washiriki usiowiana na ongezeko za dhamana za Serikali zinazouzwa.
- ii. Kuongezeka kwa upendeleo wa mabanki, ambao ndiyo washiriki wakubwa wa minada ya dhamana za Serikali, kuwekeza kwenye dhamana za Serikali kutokana pamoja na mambo mengine kuongezeka kwa mikopo chechefu.
- iii. Benki Kuu kupunguza dhamana za Serikali inazouza ili kuongeza ukwasi katika mabanki kwa lengo la kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi.

## **6. Je, dhamana za Serikali zitaendelea kuwa kivutio licha ya kushuka kwa riba?**

Dhamana za Serikali ni mojawapo ya maeneo ambayo wananchi wanaweza kuwekeza. Maeneo mengine ni kununua hisa za makapuni, kuwa na amana kwenye mabenki, na kununua rasilimali kama ardhi na majengo. Hivyo basi, mahitaji ya wawekezaji kwenye dhamana za Serikali yatategemea mwenendo wa maeneo mengine ya uwekezaji. Aidha, dhamana za Serikali zinaweza kuendelea kuwa kivutio hata kama riba itashuka kutokana na ukweli kwamba hili ni eneo salama la uwekezaji. Vilevile, mfumuko wa bei ulio chini ya kiwango cha riba ya dhamana hufanya dhamana hizo kuwa kivutio.

## **7. Kuna uhusiano gani kati ya Benki Kuu ya Tanzania na NFRA (National Food Reserve Agency) hususan kuhusu udhibiti wa mfumko wa bei kwani na wao wanatunza vyakula kwa lengo hilo?**

Benki ya Kuu ya Tanzania ni Taasisi ya umma inayotekeleza majukumu yake kwa madhumuni ya kuthibiti mfumko wa bei na kuhakikisha ustahimilivu wa mfumo wa fedha. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni taasisi ya umma pia, iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo na Ushirika iliyoungwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kutunza akiba ya chakula na kutoa chakula hicho pale kinapohitajika, hususan kunapotokea upungufu wa chakula.

Taasisi hizi za umma, japo zinafanya kazi tofauti, lakini matokeo ya kazi zake kwa pamoja yanalenga kuchangia malengo mapana ya taifa katika kuhudumia umma kwa ujumla wake. Katika msingi huu basi, inatarajiwa kuwa matokeo ya kazi za taasisi hizi hutegemeana kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano, katika kutekeleza majukumu yake wakala hutakiwa kununua chakula na kukihifadhi. Lakini, kunapotokea upungufu wa chakula, wakala husaidia kusambaza chakula kwa kuuza au kugawa kama msaada pale panapokuwa na janga la njaa. Wakala anapofanya uuzaji au ugavi wa chakula, huongeza uwepo wa chakula na hivyo kusaidia kudhibiti bei. Kanuni hii ya uhitaji na ugavi wa chakula huwa na mchango chanya kwenye jukumu la Benki Kuu la kudhibiti mfumuko wa bei.

## **8. Nini maana ya ujazi wa fedha?**

Ujazi wa fedha hujumuisha noti na sarafu zilizopo kwenye mzunguko nje ya mfumo wa kibenki pamoja na aina mbalimbali za amana zinazohifadhiwa kwenye mabenki kulingana na kiwango chake cha ukwasi. Kwa mfano:

Ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) — hii inahusisha fedha zenye kiwango cha juu kabisa cha ukwasi. Hujumuisha noti na sarafu zilizopo kwenye mzunguko nje ya mfumo wa kibenki pamoja na akaunti za amana za hundi.

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) — hii hujumuisha ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1), pamoja na amana za kawaida na zile za muda maalumu.

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) — hii hujumuisha ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2), pamoja na amana za fedha za kigeni zilizopo kwenye mabanki.

Kwa mpangilio huu wa viwango mbalimbali vya ujazi wa fedha (M1, M2, na M3); kiwango cha ukwasi cha ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) kipo juu zaidi ya kile cha M2 na M3, kwani fedha hizi huweza kutumiwa kirahisi zaidi katika kufanya malipo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kutumia fedha taslimu ama hundi ikilinganishwa na ujazi wa fedha katika tafsiri pana na pana zaidi.

**9. Je fedha zilizo katika mzunguko au miamala inayofanyika hapa nchini kupitia simu za kiganjani (mobile money) ni sehemu ya ujazi wa fedha (M3)?**

Miamala ya fedha kupitia simu za kiganjani ni sehemu ya ujazi wa fedha, na ieleweke ya kuwa miamala hii ni sehemu ya fedha zilizo katika mzunguko. Miamala hii ni sehemu ya ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na inaonyesha thamani ya malipo yaliyopitia katika mzunguko wa mitandao hiyo na siyo fedha mpya. Huduma hii inachangia kuongeza kasi ya mzunguko wa fedha katika uchumi.

**10. Benki Kuu ina malengo manne kwenye utekelezaji wa sera ya fedha, je kwa kutumia mfumo wa riba malengo mawili yaliyobaki tunayaacha?**

Tangu kupitishwa kwa Sheria ya Benki Kuu mwaka 1995, Benki Kuu ilipewa jukumu la msingi la kutunga na kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha ili kuhakikisha kunakuwepo na kiwango kidogo na tulivu cha mfumuko wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa. Sera hii ya fedha hutekelezwa kupitia udhibiti wa ujazi wa fedha. Licha ya mafanikio yaliyopatikana, sera hii imekumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo uelewa mdogo wa wananchi juu ya maana na umuhimu wa ujazi wa fedha, uwazi usioridhisha katika utekelezaji wa sera hii, mabadiliko ya teknolojia yaliyoathiri kasi ya mzunguko wa fedha na hivyo kupelekea kutotabirika kwa mahitaji ya fedha.

Hivyo basi kutokana na changamoto hizo na kwa kutambua umuhimu wa kuwa na riba ambayo itakuwa chachu ya kufikia malengo ya utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi, Benki Kuu ipo katika hatua za juu za kuanza kutumia mfumo mpya wa sera ya fedha unaolenga riba badala ya ujazi wa fedha. Chini ya mfumo huu, Benki Kuu itahakikisha kuwa riba baina ya mabenki inaendana na riba ya msingi ya Benki Kuu.

Pindi mfumo mpya wa utekelezaji wa sera ya fedha utakapoanza kutumika, kitakachobadilika ni kuacha kutumia ujazi wa fedha

taslimu kama kiashiria cha utendaji na kuanza kutumia riba za muda mfupi kama kiashiria cha utendaji katika kutekeleza sera ya fedha. Viashiria vya zamani, kama ukuaji wa fedha taslimu na ujazi wa fedha, vitaendelea kuangaliwa kama sehemu ya takwimu za utekelezaji wa sera ya fedha na havitatumika tena kwenye kusaidia maamuzi ya sera ya fedha. Viwango vya riba za muda mfupi pekee ndio vitakavyotumika kuonesha mwenendo mzima wa sera ya fedha kulingana na mwelekeo wa mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi.

## **SEHEMU YA PILI**

### **AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI**

#### **11. Unaposema akiba ya fedha za kigeni, je ni fedha halisi au raslimali? Je, zinahifadhiwa wapi?**

Akiba ya fedha za kigeni imegawanyika katika sehemu kuu mbili, yaani raslimali na fedha halisi. Raslimali hujumuisha akiba ya fedha za kigeni inayowekezwa kwenye masoko ya fedha ya kimataifa kama kwenye hati fungani za serikali za nchi zilizoendelea pamoja na za mawakala wa serikali wa nchi hizo. Vilevile, uwekezaji hufanyika kwa kuweka amana za muda maalum kwenye mabanki makubwa ya biashara duniani, Benki Kuu za nchi zilizoendelea, na mashirika ya fedha ya kimataifa. Kwa upande mwingine, fedha halisi hujumuisha akiba ya fedha za kigeni kwenye mabanki washirika kama vile Benki Kuu ya Marekani, Benki Kuu ya Uingereza, Benki Kuu ya Ufaransa, Benki Kuu ya Ujerumani na benki zingine za biashara na za kimataifa.

#### **12. Serikali hutumia mikakati gani kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni?**

Akiba ya fedha za kigeni huongezeka na kupungua katika vipindi mbalimbali vya mwaka. Akiba hizi huongezeka wakati misimu ya utalii na mauzo ya mazao mbalimbali nje ya nchi, na wakati nchi inapopokea mikopo au misaada kutoka nje. Aidha, akiba ya fedha

za kigeni hupungua endapo kutakuwa na ongezeko kubwa la malipo ya nje.

Serikali hutumia mikakati mbalimbali kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni, ikiwemo;

- i. Kuongeza thamani ya bidhaa zinazouzwa nje
- ii. Kupanua wigo wa masoko ya nje
- iii. Kuvutia wawekezaji wa nje na wa ndani ya nchi
- iv. Kufanya maboresho kwenye sekta zinazolingiziana nchi fedha za kigeni ikiwemo utalii, usafirishaji na uchukuzi
- v. Kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni

### **13. Nini athari za kiuchumi za kuwa na akiba kubwa ya fedha za kigeni.**

Nchi kuwa na akiba kubwa ya fedha za kigeni ni jambo jema kiuchumi. Akiba ya fedha za kigeni ni kinga dhidi ya athari zinazoweza kutokea endapo mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yatapungua au fedha nyingi za kigeni zitahitajika kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje. Kwa mantiki hiyo, akiba kubwa ya fedha za kigeni inasaidia nchi kulinda thamani ya sarafu yake ili kuhakikisha utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi kiujumla. Akiba kubwa ya fedha za kigeni pia huleta imani kwa wawekezaji hususan wale wa nje ya nchi kuwa mitaji yao itakuwa salama na uhakika wa malipo ya nje. Aidha, kwa kuwa na akiba ya ziada nchi inaweza kuwekeza katika masoko mbalimbali ya fedha na kujipatia faida.



## **SEHEMU YA TATU**

### **HUDUMA ZA KIBENKI**

#### **14. Wingi au uchache wa mabanki unatusaidiaje kiuchumi?**

Hadi kufikia Desemba mwaka 2018, Tanzania ilikuwa na taasisi za kibenki 62 ambazo zinajumuisha benki za biashara, benki za wananchi na taasisi nyingine za fedha ambazo zipo chini ya usimamizi wa Benki Kuu.

Kwa ujumla jukumu kubwa la mabanki ni kusaidia ukuaji wa uchumi kwa kukusanya amana za wananchi na kuwakopesha wale wanaohitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Sekta ya mabanki inatoa mchango mkubwa katika uzalishaji na ukuaji wa pato la taifa.

Benki huchangia katika uchumi wa Taifa kama kama ifuatavyo; kutunza amana, kutoa mikopo kwa sekta mbalimbali za uchumi, kutumika katika mfumo wa malipo hivyo kufanikisha miamala na kutoa ushauri na huduma nyingine za kibenki.

Hata hivyo, ili kuleta manufaa zaidi katika uchumi wa Taifa ni budi benki kuwa na mtandao mpana ili kuweza kuwafikia na kuwahudumia watu wengi. Hivyo basi, suala muhimu sio wingi wa mabanki bali ubora na ufanisi katika utoaji wa huduma.

**15. Kwa nini Serikali inauza dhamana zake kwa mabanki ya biashara? Haioni kama hiyo ndiyo sababu inayafanya mabanki hayo yasitoe mikopo kwa wananchi kwa sababu yanapata faida nzuri kutokana na ununuzi wa dhamana hizo?**

Benki Kuu kwa niaba ya serikali imekuwa ikiuza dhamana za serikali kwa lengo la kudhibiti ukwasi kwenye uchumi na kugharamia mahitaji ya kibajeti ya Serikali. Benki za biashara hununua dhamana hizo kama sehemu ya uwekezaji wao binafsi na kwa ajili ya wateja wao (makampuni na watu binafsi wasiokua na uwezo wa kununua dhamana hizo moja kwa moja kutoka sokoni).

Kwa kawaida faida ya benki za biashara hupatikana kupitia uwekezaji kwenye dhamana za serikali au mikopo kwa sekta mbalimbali za uchumi. Vigezo vinavyotumika na benki za biashara katika uwekezaji ni pamoja faida, usalama na vihatarishi vya mikopo. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha uwekezaji mwingi wa benki za biashara upo katika mikopo kwa sekta mbalimbali za uchumi na si kwenye dhamana za serikali. Hii inatokana na faida kubwa inayopatikana kutoka kwenye mikopo ya uzalishaji kuliko kwenye dhamana za serikali.

## **16. Nini hupelekea faida za mabanki kushuka?**

Kuna sababu mbalimbali zinazoweza kuathiri faida za mabanki. Miongoni mwa sababu hizo ni mikopo chechefu, kushuka kwa riba, kupungua kwa mahitaji ya mikopo, na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

## **17. Kwa nini benki za biashara hazifungui matawi katika sehemu zote za nchi zenye fursa za biashara?**

Serikali inatambua umuhimu wa wananchi wa Tanzania kupata huduma za kibenki karibu na maeneo yao. Hii imepelekea Serikali kuweka mazingira bora kupitia sera, sheria na kanuni mbalimbali, na uboreshaji wa miundombinu ili kuwezesha sekta binafsi kuanzisha mabanki na kutoa huduma bora kwa wananchi. Vilevile, Serikali imekuwa ikihamasisha na kuyasisitiza mabanki umuhimu wa kupeleka huduma za kibenki karibu na wananchi. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali, wadau wa sekta ya fedha wamebuni namna mbadala za kufikisha huduma za kifedha kwa wananchi ikiwemo, mawakala wa benki na huduma za kibenki kwa njia ya simu. Jitihada zote hizi, ingawa hazijamaliza tatizo, kwa kiasi kikubwa zimesaidia kusogeza huduma za kibenki karibu na wananchi.

## **18. Huduma za Wakala wa Mabenki zinawasaidiaje Watanzania?**

Pamoja na jitihada za mabenki kutoa huduma za kifedha, kulikuwa na changamoto ya kuyafikia baadhi ya maeneo kutokana na gharama za kufungua matawi katika maeneo hayo. Hii ilisababisha kubuni namna mbadala ya kutumia mawakala ili kufikisha huduma katika maeneo mbalimbali, hasa ambayo yalikuwa hayajafikiwa, kwa gharama nafuu. Huduma za wakala wa mabenki zimewezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma za kibenki na kuwapunguzia gharama ya kusafiri umbali mrefu kupata huduma.

Huduma ambazo zinazotolewa na mawakala zinajumuisha kuweka na kutoa amana, kupokea na kulipa mikopo, kutuma fedha, kuuliza salio na kupata taarifa fupi za akaunti. Pia mawakala hucusanya taarifa na nyaraka kwa ajili ya kufungua akaunti, kuomba mikopo, kadi ya benki na huduma nyingine zinazoruhusiwa.

## **19. Serikali inanufaikaje na utoaji wa huduma za kibenki kwa njia ya simu (mobile banking)?**

Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaomiliki simu za kiganjani na ubunifu wa watoa huduma za kifedha kulisababisha uanzishwaji wa huduma za kibenki kwa njia ya mtandao wa simu. Jambo hili limekuwa na tija kwa watumiaji na watoa huduma za kifedha pamoja na Serikali. Baadhi ya faida ambazo Serikali inapata kutokana na huduma hizi ni kama ifuatavyo:

- i. Usalama wa malipo: Huduma za malipo kwa njia ya mitandano ya simu ni salama kuliko malipo ya fedha taslimu. Mathalani, tangu Serikali imeanza kukusanya kodi kwa njia ya mtandao wa simu imeweza kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika makusanyo;
- ii. Uharaka na uhakika: Huduma za fedha kwa njia ya mtandao wa simu pia zimeweza kuhamasisha wananchi kulipa kodi na tozo mbalimbali kwa haraka na uhakika pasipo kulazimika kufika katika ofisi husika. Kwa malipo haya, Serikali inakuwa na uhakika wa kupata mapato yake haraka na kwa uhakika zaidi;
- iii. Kupunguza gharama za ukusanyaji wa mapato: Hii inatokana na matumizi ya teknolojia na uhitaji mdogo wa raslimali watu katika zoezi la ukusanyaji, hivyo kupunguza matumizi yasiyo ya lazima

## **20. Tanzania inafaidika vipi kupitia matumizi ya kadi za benki za malipo?**

Kadi za benki za malipo zina matumizi na faida mbalimbali. Kadi hizi hurahisisha upatikanaji wa fedha katika machine za fedha (ATMs), hurahisisha malipo kwenye mashine za malipo (Point of Sales), hurahisisha malipo kwenye mtandao (e-commerce), hupunguza ubebaji wa fedha taslimu, na huwezesha kupatikana kwa taarifa za matumizi ya mtumiaji. Aidha, wananchi wanaosafiri nje ya nchi na wageni wanaokuja Tanzania hufaidika kwani huweza kutumia kadi

hizo badala ya kusafiri na fedha taslimu na kuwahakikishia usalama wa fedha zao. Vilevile, matumizi ya kadi hizi hupunguza gharama za kuchapisha pesa na kuongeza kasi ya mzunguko wa fedha katika uchumi.

## **21. Benki Kuu inadhibiti vipi shughuli za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni?**

Maduka yote ya kubadilishia fedha za kigeni Tanzania Bara na Visiwani yanaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za maduka ya kubadilishia fedha za kigeni ya mwaka 2008 na marejeo yake ya 2017, zilizowekwa kwa mujibu wa ibara ya 5(a) na 7 (1) ya Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992. Ili kudhibiti shughuli za maduka ya kubadilisha fedha, yafuatayo ni miongoni mwa masharti yaliyoainishwa kwenye sheria na kanuni tajwa hapo juu:

- i. Maduka ya fedha za kigeni yanatakiwa kuweka kumbukumbu za mauzo na manunuzi kwenye nukushi 'computer' na kutoa stakabadhi inayochapishwa kutoka kwenye nukushi kwa kila muamala utakaofanyika;
- ii. Maduka ya fedha za kigeni hayaruhusiwi kuuza kiasi kinachozidi dola za Kimarekani elfu kumi au kiasi kama hicho katika aina nyingine ya fedha za kigeni kwa mteja mmoja kwa mara moja;
- iii. Katika kuhakikisha uzingatiaji wa masharti haya, Benki Kuu imeweka utaratibu wa kutoa leseni kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja, na duka lolote litakalokuwa

limefanya kinyume na matakwa ya kanuni na sheria halitapewa leseni kwa kipindi cha mwaka unaofuata.

Ili kusimamia sheria na kanuni tajwa hapo juu, wakaguzi kutoka Benki Kuu kwa kushirikiana na vyombo vya sheria hufuatilia uendeshaji wa maduka ya fedha za kigeni na wale wanaokwenda kinyume cha taratibu hupewa maelekezo na adhabu mbalimbali

## SEHEMU YA NNE

### USIMAMIZI WA MABENKI

**22. Inapotokea benki imefilisika, wateja wenye amana kubwa hurejeshewa kiasi kidogo cha amana zao. Nini maelezo yake?**

Benki au Taasisi ya Fedha yenye leseni ya Benki Kuu inapofungwa kwa kufilisika au kwa kutokidhi masharti na kuwekwa chini ya ufilisi, upo utaratibu uliowekwa mahsusi kuhakikisha kuwa wateja wote wenye amana kwenye taasisi hizo wanarejeshewa fedha zao. Hata hivyo, wateja wenye amana kubwa hulipwa kwa awamu.

Kwa mujibu wa taratibu za bima ya amana, kiwango cha juu cha fidia ya awali ni Shilingi Milioni Moja na Laki Tano (1,500,000/-). Ukomo huu umezingatia miongozo iliyowekwa na umoja wa taasisi zinazotoa bima ya amana (International Association of Deposit Insurers) na uwezo wa mfuko. Kiwango hiki kina uwezo wa kulipa fidia kwa asilimia kubwa ya wenye amana katika mabenki. Hata hivyo, kiwango hicho hufanyiwa marejeo kwa lengo la kuboresha. Malipo ya awamu nyingine, hasa kwa wateja wenye amana kubwa, hufanyika yanapopatikana makusanyo ya mali za benki/taasisi ya fedha iliyofungwa ili kulipa wadai kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi.



### **23. Benki Kuu ya Tanzania inazisimijaje pesa zilizoko kwenye mitandao ya simu (mobile money)?**

Pesa zilizoko kwenye mitandao ya simu huwekwa kwenye akaunti maalumu ya dhamana (Trust Account) katika mabenki. Akaunti hiyo huwekwa pesa ambayo inapatikana katika miamala ya simu tu. Hivyo, pesa ya kielektroni iliyoko kwenye mitandao ya simu hutakiwa kuwa sawa na pesa iliyoko kwenye akaunti ya dhamana.

Katika kusimamia mifumo hii ya malipo kwa njia ya simu, Benki Kuu kupitia vifungu vyake vya sheria ya mifumo ya malipo ya mwaka 2015 huwataka watoa huduma kwa mitandao ya simu na mabenki kuwasilisha ripoti ya fedha ili kujiridhisha kuwa kiasi cha pesa kilichowekwa kwenye akaunti ya dhamana ni sawa na kile kilichoko kwenye mitandao ya simu ili kuhakikisha usalama wa fedha katika mfumo husika wa malipo.

### **24. Usimamizi wa mabenki na uandaaji wa sera ya fedha, je unahusisha mabenki binafsi?**

Benki Kuu ya Tanzania ndicho chombo chenye dhamana ya kusimamia mabenki yote nchini, kuandaa na kutekeleza sera ya fedha kwa ajili ya ustawi wa uchumi wa nchi. Kwa ujumla sera ya fedha haibagui mtu wala taasisi yeyote. Uandaaji wa sera hii ya fedha unahusisha wadau mbalimbali wa uchumi kama vile Serikali, taasisi za kifedha, na wadau wengine kutoka sekta binafsi.

## **SEHEMU YA TANO**

### **VIWANGO VYA RIBA**

**25. Nini huchangia riba za mikopo kupanda? Je benki za biashara hutumia vigezo gani kuweka riba zake katika mikopo?**

Ikumbukwe kwamba Serikali chini ya mfumo wa soko huria iliacha kupanga bei ya bidhaa mbalimbali, ikiwemo riba inayotozwa na mabenki. Katika mfumo wa soko huria bei zinaamriwa na soko kutokana na mahitaji na ugavi. Katika mazingira haya, riba huamriwa kati ya mabenki na taasisi nyingine za kifedha kwa upande mmoja na wateja kwa upande mwingine. Vigezo vinavyotumika na mabenki kupanga riba zinazotoza kwenye mikopo ni pamoja na gharama za mitaji; kiasi cha ukwasi ilichonacho; gharama za uendeshaji; matarajio ya mfumuko wa bei; na kiwango cha vihatarishi vinavyotokana na biashara ya kukopesha, kama vile uwezekano wa mkopaji kutorejeshwa mkopo, ubora wa dhamana na historia ya mkopaji.

**26. Benki Kuu huchukua hatua zipi dhidi ya riba kubwa zinazotozwa na mabenki?**

Endapo itaonekana kuwa viwango vya riba vinapanda kwa kasi kwa sababu ya upungufu wa ukwasi wa mabenki, Benki Kuu huchukua hatua ya kuongeza ukwasi kwa kutumia njia mbalimbali. Hatua

nyingine ni kwa kudhibiti mfumuko wa bei kwani ni kigezo kimojawapo cha msingi katika kukokotoa riba za mabenki. Pia, Benki Kuu inazitaka benki kuweka wazi viwango vya riba za amana na mikopo ili kuwaweza wateja kufanya maamuzi sahihi.

Benki Kuu pia inazitaka taasisi zote za kifedha kuwasilisha na kutumia taarifa za wakopaji kwenye/kutoka kwenye mfumo wa kuhifadhi taarifa za wakopaji (**Credit Reference Bureaux**). Vilevile, Benki Kuu hutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya sekta ya fedha.

## **27. Kwa nini watanzania wengi wakienda kukopa kwenye mabenki wanaambiwa hawakopesheki?**

Ushindani katika sekta ya kibenki umeongezeka, hali inayopelekea kuongezeka kwa uhuru wa wateja kuchagua mkopeshaji atakayekuwa anakidhi mahitaji yao pamoja na unafuu wa gharama za mikopo. Kukopesheka kwa mteja hutegemea makubaliano baina ya mteja na benki husika.

## **28. Benki Kuu inafanya juhudi gani ili kuhakisha wanachi wa kawaida wanafadika na huduma za mikopo inayotolewa na benki za kibiashara?**

Benki Kuu inatambua kuna vikwazo kwa wananchi wa kipato cha chini kunufaika na huduma za mikopo zinazotolewa na mabenki. Hii

inatokana na kutokidhi vigezo na masharti ya kupewa mikopo, hususan dhamana, kwa sababu wananchi wengi wanajihusisha na sekta isiyo rasmi, na dhamana zao pia sio rasmi. Hili ni suala pana na linahitaji ushirikiano na taasisi nyingine za serikali ili kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kuwa na dhamana zinazokubalika na mabanki hasa hati miliki ya ardhi.

Hivyo, Benki kuu inaendelea kuzisimamia benki za biashara ili ziendelee kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na utaratibu. Vilevile, Benki Kuu inalo dawati la kushughulikia migogoro baina ya Benki za Biashara na wateja wao ili kuwanufaisha watumiaji wa huduma za kibenki.

## **29. Gharama za huduma za kibenki zinawaumiza sana wananchi. Benki Kuu ina maoni gani?**

Benki Kuu ya Tanzania haiingilii gharama zinazotozwa na mabanki kwa wateja wake, gharama hizi zinaamuliwa na soko. Hata hivyo, Benki Kuu imeziagiza benki zote kuweka wazi gharama zao za huduma, ikiwa ni pamoja na kwenye kumbi zao za benki ili kila mteja aweze kujua gharama ambazo atatozwa kwa huduma anazoomba kutoka kwa benki husika. Kwa hiyo tunawashauri wateja wote wa mabanki kujua na kuuliza gharama za huduma mbalimbali zinazotolewa na mabanki kabla hawajaingia makubaliano yoyote na benki hizo. Endapo kutakuwa na mgogoro baina ya benki za

biashara na wateja wao, Benki Kuu imeanzisha dawati maalumu kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya aina hiyo.

### **30. Pengo kati ya riba inayolipwa kwa fedha zinazowekwa benki na riba inayotozwa kwenye mikopo inayotolewa na benki.**

Itakumbukwa kuwa biashara ya mabanki iliwekwa huru mwaka 1991 ilipopitishwa Sheria ya Usimamizi wa Mabanki na Vyombo vya Fedha ya Mwaka 1991 [Banking and Financial Institutions Act, 1991] iliyokuja kuboreshwa mwaka 2006. Sambamba na sheria hii, mabanki binafsi yamepewa nafasi ya kupanga riba za huduma inayotolewa kulingana na mazingira ya kiuchumi ambayo ni ya ushindani. Lengo la kuweka ushindani katika sekta ya fedha ni kuhakikisha kwamba huduma za kibanki zinatolewa kwa wateja kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

Pengo kati ya riba inayolipwa kwa amana na riba za mikopo inayotolewa na mabanki limekuwa likipungua mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2017 kwa wastani pengo hilo lilikuwa limepungua na kufikia asilimia 7.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.9 mwaka 2000. Kupungua kwa pengo hilo kunatokana na hatua mbalimbali ambazo Serikali na Benki Kuu zimeendelea kuchukua. Hatua hizo ni pamoja na kuweka mazingira bora ya kibiashaara na kiushindani, na kudhibiti ukwasi.

## SEHEMU YA SITA

### THAMANI YA SHILINGI

#### **31. Kwa nini Serikali kupitia Benki Kuu haizuii matumizi ya fedha za kigeni na kuisisitiza matumizi ya shilingi ya Tanzania?**

Mwaka 2017, Serikali ilitoa tamko rasmi kuhusu matumizi ya fedha za kigeni kulipia bidhaa na huduma katika soko la ndani. Katika tamko hilo, Serikali iliagiza kuwa bei zote nchini zitangazwe kwa Shilingi ya Tanzania zikijumuisha kodi za nyumba za kuishi na maofisi, bei ya ardhi, gharama za elimu na afya, bei za vifaa vya kielektroniki n.k.

Aidha, tamko hilo lilieleza kuwa bei ambazo wateja wake ni watalii au wateja wasio wakazi zinaweza kutangazwa kwa pesa za kigeni na malipo yake yanaweza kufanywa kwa Shilingi ya Tanzania au fedha za kigeni. Malipo haya yanajumuisha malipo ya gharama za mizigo bandarini kwenda nchi za nje, gharama za huduma katika viwanja vya ndege na viza kwa wageni, gharama za hoteli kwa watalii n.k. Viwango vya kubadilisha pesa hizo vitakavyotumika kupanga bei viwe wazi na visizidi vile vya soko. Vile vile watakaopata huduma hiyo watambuliwe kwa vitambulisho vyao kama hati za kusafiria na nyaraka za usajili wa kampuni. Tamko hili linatamka wazi kuwa mkazi yeyote wa Tanzania asilazimishwe kulipia bidhaa au huduma yoyote hapa nchini kwa fedha za kigeni.

Ni vyema pia ikafahamika kuwa, Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, sehemu ya tatu, kipengele cha 26, imeweka wazi kuwa Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo ya bidhaa na huduma nchini, (yaani legal tender). Hii ina maana kwamba ni kosa kwa mtu yeyote kukataa kupokea Shilingi ya Tanzania kwa malipo halali nchini, au kushurutisha mkazi yeyote wa Tanzania kufanya malipo yoyote kwa fedha za kigeni. Hivyo kanuni zipo na Benki Kuu inazisimamia kisheria kabisa, na kama zinakiukwa ni suala la ushirikiano kati ya wananchi na vyombo vya sheria kuchukua hatua. Mtanzania yeyote atakayelazimishwa kulipia bidhaa au huduma kwa fedha za kigeni bila hiari yake, atoe taarifa kwa wahusika ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Pamoja na maelezo haya, ni vyema izingatiwe kwamba Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 na Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 1998, zinatamka bayana kwamba Watanzania wanaruhusiwa kupokea, kumiliki, na kutumia fedha za kigeni kwa shughuli zao za kiuchumi hapa nchini. Ruhusa hii ilikuwa na nia njema kwa uchumi wa nchi yetu na sio kuyumbisha thamani ya sarafu au kuleta madhara ya aina yeyote ile. Kwa kuboresha upatikanaji wa fedha za kigeni, na kuwahamasisha wale waliokuwa nazo nje wazirejeshe nchini na kuzitumia bila woga ndio kumeendelea kusaidia utulivu tulio nao kwenye soko letu la fedha za kigeni. Ni vyema basi wananchi ikijumuisha wafanyabiashara na

watoa huduma wote nchini wazingatie maelekezo ya Serikali kwa kutekeleza Sheria zilizopo.

### **32. Benki Kuu inafaidika vipi na shughuli zinazoendeshwa na maduka ya kubadilisha fedha?**

Uwepo wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini umesaidia udhibiti wa soko haramu la kuuza na kununua fedha za kigeni na pia yamerahisisha upatikanaji wa fedha za kigeni kwa wananchi bila kupitia Benki Kuu kama ilivyokuwa awali. Aidha, uwepo wa maduka haya umesaidia kupatikana kwa takwimu sahihi za fedha za kigeni zinazoingia na kutoka nchini, pamoja na madhumuni ya ununuzi.

### **33. Thamani ya Shilingi ya K Tanzania imezidi kuporomoka dhidi ya Dola ya Marekani. Je Benki Kuu ya Tanzania inafuata utaratibu gani wa kuimarisha shilingi?**

Thamani ya shilingi yetu huwekwa na soko (yaani ugavi na uhitaji wa fedha za kigeni). Zipo sababu nyingi za msingi zinazosababisha thamani ya shilingi kupungua, mojawapo ikiwa ni mapato madogo yatokanayo na uuzaji wa huduma na mazao yetu ya biashara nje ya nchi na gharama/thamani kubwa ya bidhaa na huduma zinazoagizwa toka nje ya nchi, ikiwemo mitambo na bidhaa nyingine za uwekezaji. Vilevile, kiwango cha mfumuko wa bei hapa Tanzania kinapokuwa juu ukilinganishwa na viwango katika nchi tunazofanya nazo biashara inaweza kupelekea kuyumba kwa sarafu ya Tanzania



kwani huzifanya huduma na bidhaa zetu kwenye soko la dunia zinapopimwa kwa thamani ya fedha za kigeni kuwa aghali na kupelekea kupungua kwa mauzo nje ya nchi. Hali hii pia huzifanya huduma na bidhaa toka nje ya nchi kuwa rahisi na kuchochea ununuzi wa bidhaa toka nje. Uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje ya nchi wenye thamani kuliko mapato nchi inayoyapata kwa kuuza bidhaa na huduma nje ya nchi husababisha nakisi katika urari wa biashara ya nje ya nchi. Kadiri nakisi hii inavyoongezeka, uimara wa sarafu ya nchi hupungua.

Ili kudumisha uimara na utulivu wa shilingi ya Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania inahakikisha mfumuko wa bei nchini unakuwa mdogo na tulivu. Sarafu imara na tulivu inasaidia kuchochea mauzo nje ya nchi, hivyo kuimarisha uwiano wa sarafu ya Tanzania na sarafu za nchi nyingine.

Ifahamike kwamba si kila mara thamani ya shilingi inapopungua kuna madhara kwenye uchumi na maisha ya watu kwani ingawa bei za bidhaa toka nje huongezeka, bei za huduma na mazao yetu kwenye soko la dunia zinapopimwa kwa thamani ya fedha za kigeni hupungua, na hivyo kumpa Mtanzania anayeuzi nje ushindani zaidi katika soko la kimataifa.

Hali kadhalika, Shilingi yenye nguvu huzifanya bidhaa toka nje ya nchi kuwa rahisi hivyo basi kushawishi uagizaji wa bidhaa toka nje. Hali hii siyo nzuri kwa viwanda vya ndani kwani inaweza kudumaza

ushindani wa bidhaa za viwanda vya ndani kutokana na bei nafuu ya bidhaa za nje. Pia, shilingi yenye nguvu huweza kuzifanya bidhaa zetu tunazouza nje ya nchi ghali na kudidimiza uuzaji wa bidhaa zetu nchi za nje hivyo kumwathiri mkulima wa mazao ya biashara. Ni vyema ieleweke kwamba, ufumbuzi wa kudumu wa kutengamaa kwa thamani ya shilingi kutategemea zaidi kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya nje na hali ya viashiria vya uchumi vya nchi tunazofanya nazo biashara.

#### **34. Kwa kuwa mauzo ya madini na vito vya thamani yanaingiza fedha nyingi za kigeni, kwa nini fedha hizo haziimarishi sarafu ya Tanzania?**

Ili fedha za kigeni zitokanazo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi ziweze kuimarisha sarafu ya Tanzania ni lazima ziweze kukidhi mahitaji yetu ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje. Hata hivyo, sehemu ndogo tu ya mapato ya fedha za kigeni yanayotokana na madini imekuwa ikirejeshwa nchini na wawekezaji. Hii inatokana na wawekezaji kulazimika kulipa madeni yao waliyokopa kwenye mabanki nje ya nchi, mapungufu yaliyokuwepo katika mikataba ya uwekezaji, na mfumo mzima wa uzalishaji na uuzaji wa madini na vito vya thamani.

Mwaka 2017, Serikali ilianza kupitia upya mikataba ya madini na wawekezaji pamoja na kuongeza usimamizi wa mfumo mzima wa uchimbaji na uuzaji madini ili fedha nyingi za kigeni ziweze kuingia

nchini na kuimarisha sarafu ya Tanzania. Zoezi hili lilikamilika kwa kupatikana kwa sheria mpya ya madini na kanuni zake. Ni matumaini yetu kuwa mageuzi haya yataongeza tija itokanayo na uchimbali na bishara ya madini nchini, hivyo kuchangia uimara wa fedha yetu.

### **35. Ukomo wa Dola za Marekani 10,000 uliowekwa na Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 imepitwa na wakati?**

Ukomo wa dola za Marekani 10,000 uliowekwa kwenye sheria ya fedha za kigeni ya mwaka 1992 ulikusudia kuzuia vitendo vya kihalifu vinavyoweza kusaidiwa na matumizi makubwa ya fedha taslimu kama vile utakatishaji wa fedha haramu pamoja na kufadhili ugaidi. Ukomo huu pia unasaidia kuzuia matumizi makubwa ya fedha nje ya mfumo wa kibenki. Kutokana na kuwepo kwa uhuru wa kuuza na kununua bidhaa na huduma nje ya nchi mtu yeyote anaruhusiwa kuagiza kutoka nje bidhaa na huduma za thamani yoyote ilimradi asivunje sheria. Malipo makubwa ya manunuzi kutoka nje yanatakiwa yafanyike katika mfumo wa kibenki ambao zaidi ya kuzuia uhalifu unawezesha ufuatiliaji wa takwimu sahihi za biashara ya nje.

### **36. Je, kuna faida au hasara gani kwa nchi kutumia sarafu za aina mbili kwa wakati mmoja?**

Fedha huwa na matumizi makubwa matatu; kuuza na kununua bidhaa na huduma; kuhifadhi thamani na kukokotoa bei. Nchi moja inapotumia sarafu ya nchi nyingine sambamba na matumizi ya sarafu yake kuna faida na hasara kadhaa zinazoweza kujitokeza.

Hasara zitokanazo na nchi kutumia sarafu ya nchi nyingine katika kununua na kuuza bidhaa na huduma ni pamoja na:

- i. Kushuka kwa ufanisi na uhuru katika utekelezaji wa sera ya fedha kwani pale pesa hiyo ya kigeni itapopungua kwenye mzungungo wa fedha, kwa sababu yoyote ile, ujazi wa fedha nao hupungua. Na ikitokea fedha hiyo ya kigeni ikaingia nchini kwa wingi ujazi wa fedhaa huongezeka na kuipa kazi ya ziada Benki Kuu kuhakikisha kuwa kuna utulivu wa bei.
- ii. Nchi hupunguza faida inayotokana na kuwa na pesa yake yenyewe inayochagizwa na watu kutumia sarafu ya nchi husika. Katika mazingira ambayo sarafu ya kigeni ndiyo inayotumika zaidi faida hiyo huenda kwa nchi ya kigeni.

- iii. Kupungua kwa faida ya nchi kuwa na sarafu yake yenyewe kunaweza kupunguza uwezo wa Benki Kuu wa kuzikopesha benki za biashara ili kuhakikisha uwepo wa uthabiti wa sekta ya fedha.

Utaratibu huu kwa upande mwingine unasaidia kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha na mfumuko wa bei unaotokana na Benki Kuu kuikopesha Serikali ya nchi husika kugharamia matumizi yake.

### **37. Paundi ina nguvu lakini dola inatumika zaidi kwenye biashara, tofauti ni nini? Sielewi ni kwa nini tunaiheshimu sana dola**

Paundi ya Uingereza na dola ya Marekani zote ni fedha ambazo zinatumika kwa biashara za kimataifa na pia kama akiba ya fedha za kigeni. Sarafu hizi mbili zikiangaliwa kwa thamani dola ni ndogo kuliko paundi mfano kwa mwaka 2018 unahitaji takriban dola 1.3 kupata pauni 1. Hata hivyo kinachosababisha fedha itumike zaidi sio udogo au ukubwa wake kithamani ila ni jinsi inavyokubalika katika biashara za kimataifa. Sababu nyingine inayofanya dola ya Marekani ikubalike zaidi ni historia ya uchumi wa Marekani. Kwa miaka mingi uchumi wa Marekani ulikuwa zaidi ya mara mbili ya uchumi wa nchi inayofuatia kwa ukubwa duniani kiuchumi. Kwa mfano mwaka 2017 uchumi wa Marekani ulikadiriwa kuwa dola za Marekani trilioni 19 ukifuatiwa na uchumi wa Jumuiya ya Ulaya

ambao ulikadiriwa kuwa dola za Marekani trilioni 17. Kutokana na historia yake dola imekubaliwa na kuaminiwa zaidi duniani kote.

### **38. Kwa nini kiwango cha kuuza dola katika benki za biasharani kidogo kuliko kile kilichopokatika maduka ya kubadilisha fedha?**

Mabenki ya biashara yana vyanzo vingi zaidi vya kununua fedha za kigeni kuliko maduka ya kubadilisha fedha. Mabenki ya biashara yanaweza kununua fedha kutoka soko la jumla la fedha za kigeni kati ya mabenki. Katika soko hili mabenki yanapata fedha za kigeni kwa bei ya chini kwa sababu ni soko la jumla. Soko hili linakidhi sehemu kubwa ya mahitaji ya mabenki ya fedha za kigeni. Maduka ya kubadilisha fedha kwa upande mwingine hayana fursa kama hii, chanzo chao kikubwa cha fedha za kigeni ni wageni wanoingia nchini na fedha hizo, ambao baadhi yao pia huzipeleka kwenye mabenki ya biashara kufungua akaunti za amana. Kutokana na mfumo huu, ni lazima maduka ya kubadilisha fedha yajaribu kuvutia wateja kwa kuwapa bei nzuri.

leleweke pia, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yapo mengi katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Hali hii inasaidia kuleta ushindani katika bei na kumfanya mtu yeyote mwenye fedha za kigeni kuzibadili na kupata shilingi za Kitanzania kwa urahisi na katika sehemu ambayo anaona anapata kiwango kizuri cha ubadilishaji.

### **39. Kuna Mikakati gani ya uboresha uzalishaji wa ndani (Import substitution industries)**

Mikakati ya uboresha uzalishaji wa ndani inatekelezwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- i. Matumizi ya raslimali za ndani
- ii. Viwanda vya kuzalisha bidhaa zinatumiwa na watu wengi (mass consumption)
- iii. Viwanda vinavyotoa ajira nyingi.

Hata hivyo mikakati hii haikinzani na ule mkakati mama wa kuanzisha viwanda vya msingi kama vile viwanda vya chuma na gesi.

## SEHEMU YA SABA

### UTANGAMANO WA KIUCHUMI

**40. Hivi sasa kuna mchakato wa kuanzisha sarafu moja kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sisi Tanzania tutaathirika vipi? Ni utaratibu gani unatumika katika kuanzisha sarafu moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki? Katika kuelekea uanzishaji wa Sarafu moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wake na viashiria vilivyopo?**

Mchakato wa kuanzisha Umoja wa Fedha unaolenga kuanzishwa kwa sarafu moja kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulianza Januari 2011 wakati majadiliano kati ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuandaa Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha yalipoanza rasmi. Majadiliano hayo yalikamilika mwezi Julai 2013 na Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha kupitishwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 28 Novemba 2013 na kusainiwa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya tarehe 30 Novemba, 2013. Itifaki hiyo iliridhiwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili utekelezaji uanze maramoja.

Ili kutimiza dhumuni kuu la Umoja wa Fedha la kujenga ukanda tulivu wa kifedha (monetary and financial stability zone)



utakaorahisisha na kusaidia ukuaji wa biashara na shughuli za kiuchumi ndani ya Jumuiya, Nchi Wanachama zimekubaliana: kuunda Benki Kuu ya Jumuiya itakayosimamia sera moja ya fedha na sera moja ya viwango vya ubadilishanaji fedha za kigeni; kuongeza kiwango na kasi ya mtangamano wa masoko ya fedha na mitaji; kuwa na kanuni za aina moja/zinazoshabihiana za kusimamia sekta ya fedha; kuwa na utaratibu wa kuendesha shughuli za uchumi bila kukinzana na malengo ya Umoja wa Fedha; na kuanzisha sarafu moja kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hata hivyo, Umoja wa Fedha utanzishwa hatua kwa hatua kwa kuzingatia mpango kazi ulioandaliwa, pamoja na Nchi Wanachama kufikia vigezo vilivyokubalika vya muunganiko wa uchumi mpana na masharti mengine yaliyoainishwa katika Itifaki hususan kutekeleza kikamilifu itifaki za ushuru wa forodha na soko la pamoja na urazinishaji (harmonization) wa sera za fedha, takwimu, usimamizi wa mabengi na mifumo ya malipo. Hatua ya mwisho kabisa ni uanzishwaji wa sarafu moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayotarajiwa kuanzishwa mwaka 20124.

Faida itakayopata Tanzania kutokana na Umoja wa Fedha na hasa kuwepo kwa Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na:

- i. Kupunguza gharama za kufanya biashara katika nchi Wanachama na hivyo kuhamasisha ukuaji wa biashara baina ya Nchi Wanachama na ukuaji wa uchumi kwa ujumla;
- ii. Kwa Kuwa na sarafu moja, Umoja wa Fedha utaepusha athari za ubadilishanaji wa fedha ndani ya Jumuiya;
- iii. Kuwezesha nchi Wanachama kuwa na kiwango kidogo na tulivu cha mfumuko wa bei;
- iv. Kuwezesha nchi Wanachama kuwa na viwango vidogo vya riba vya kukopa; na
- v. Kutumia sarafu moja kutaleta uwazi katika bei na hivyo kuongeza ushindani wa soko ndani ya Jumuiya.

Pamoja na manufaa haya, zipo changamoto zitakazojitokeza kutokana na kujiunga na Umoja wa Fedha ikiwa ni pamoja na kupoteza uhuru wa kutumia sera ya fedha na ile ya ubadilishanaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya kujikinga na madhara ya kiuchumi ambayo yanaweza kuathiri uchumi wetu. Hata hivyo, kutokana na kushabihiana kwa uchumi wa nchi za Afrika Mashariki, athari za kiuchumi zitakuwa zinafanana na hivyo zitadhibitiwa na Benki Kuu ya Afrika Mashariki.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa viashiria vya uchumi kuelekea sarafu moja ambapo:

- i. Mfumuko wa bei umekuwa chini ya ukomo uliowekwa na jumuiya ya Afrika mashariki wa asilimia 8

- ii. Nakisi ya bajeti ya Serikali inayojumisha misaada imeendelea kuwa chini ya ukomo uliowekwa wa asilimia 3
- iii. Deni la Serikali limeendelea kuwa chini ya ukomo uliowekwa wa asilimia 50
- iv. Hazina ya fedha za kigeni imeendelea kuwa juu ya lengo lilowekwa la miezi 4.5

## SEHEMU YA NANE

### SARAFU

**41. Dunia imekuwa ikienda kwa kasi halikadhalika utandawazi pamoja na mifumo ya fedha ya kidijitali ambayo haiwezi kuiacha Tanzania Nyuma kama vile sarafu ya kidijitali ya Bitcoin: -Je, Serikali ina mtazamo gani kuhusu Bitcoin?**

‘Cryptocurrency’ ni sarafu ya ya kidigitali iliyoungwa kiteknolojia (cryptographic) ili kuwa salama, na mara nyingi katika mazingira yasiyojulikana (unknown identity). Sarafu hii inatumika kwenye mtandao tu na hutumia mifumo ya msimbo (coding) ambayo sio rahisi kuihujumu. Teknolojia inayotumika katika kutengeneza na kusambaza cryptocurrency inajulikana kama ‘blockchain’ (distributed ledger). Mfumo huu unatumia itifaki ambayo inathibitisha miamala bila kuhitaji mtu au taasisi ya kati (peer-to-peer validation protocol) na kujikagua yenyewe (self-audit). Hivyo mfumo huu unajisimamia wenyewe na haudhibitiwi na mamlaka yoyote. Aidha, inaelezwa kuwa mfumo hauna udhaifu inayoweza kusababisha kushindwa.

Cryptocurrency ya kwanza ilikuwa Bitcoin, ambayo iliundwa mwaka 2009 na ndiyo ambayo bado inajulikana zaidi kuliko nyingine. Kumekuwa na usambaaji wa Cryptocurrency mbalimbali katika muongo uliopita na mpaka sasa kuna zaidi ya 1,600 zilizopo kwenye mtandao.

## **a. Mambo ya Msingi Kuhusu Cryptocurrency**

Kutokana na utafiti na uchambuzi uliofanyika, yafuatayo ni mambo ya msingi yanayohusu Cryptocurrency:

- i. Mtandao wa Blockchain unafanya kazi katika hali ya makubaliano baina ya watumiaji na ukilinganisha taarifa moja kwa moja na vitalu vingine kila baada ya dakika kumi. Ina mfumo wa ukaguzi wa kujitegemea wa miamala ya kidigitali. Mtandao huu unalinganisha na kupatanisha kila mihamala inayofanyika.
- ii. Inadhaniwa pia teknolojia hii inaweza kuongeza ufanisi na kupunguza gharama kuwezesha uandikaji wa mikataba rahisi ambayo inaweza kutekelezeka katika mazingira maalum.
- iii. Wafuasi wa teknolojia hii wanaona na wanasema kwamba Blockchain inaruhusu mihimili ya utawala kuwa wazi zaidi na kuthibitishwa wakati wa kusimamia mali, vitegauchumi na taarifa zilizo katika mfumo wa kielektroniki.

## **b. Changamoto kuhusu Cryptocurrency**

Dhana ya sarafu ya kidigitali ni mpya sana, na Benki kuu nyingi ulimwenguni pote bado wanafuatilia kwa karibu na kufanya utafiti kuhusu matokeo ya teknolojia hiyo. Ubunifu mpya katika sekta ya huduma za fedha zinazotumia teknolojia unaonyesha kwamba

unaweza kuboresha hali ya sasa, lakini pia kuendeleza dhana ya fedha za kidigitali, na kuifanya mgombea halisi kuchukua nafasi ya fedha zinazotolewa na Benki Kuu, kama ilivyo sasa. Hali hii inaweka serikali za dunia kwenye nafasi isiyo ya kawaida ambayo haijawahi kufikirika.

Hatari zinazokabiliwa na kanuni za usimamizi wa fedha ziko katika aina mbili; kwa upande mmoja, kuunda sheria inayohimiza kupitishwa kwa miundombinu ya kifedha inaweza kuwa chanzo kikubwa cha ushindani wa kiuchumi; kwa upande mwingine, kuwapa watu uhuru mkubwa kunaweza kuharibu uaminifu wa pesa za karatasi za nchi. Usawa kwenye swala hili bado haujafikiwa, na kwa hiyo, serikali kuu zimechukua hatua zinazotofautiana kabisa katika kushughulikia kuanzishwa kwa Bitcoin (na teknolojia nyingine za cryptocurrency) katika nchi zao.

Hii imetokana na changamoto zifuatazo:

- i. Mazingira ya usiri yanayohusisha teknolojia ya blockchain hasa katika Bitcoins. Kuna maswali machache ya msingi ambayo hayawezi kujibiwa (kwa mfanno: kutojulikana kwa aliyeyumba bitcoins). Hali hii inaongeza hatari katika udhibiti katika suala la kuruhusu au kukuza teknolojia.
- ii. Kutozingatia mahitaji ya Utakatishaji wa fedha haramu (Antimoney laundering (AML)/ Combating Financing of Terrorism (CFT)) – hii inatokana na usiri unaozunguka

teknolojia hii unaosababisha kutojulikana kwa mnunuzi na mwuzaji kwa vyombo vya usimamaizi wa biasahara.

- iii. Kutodhibitiwa na Chombo chochote Duniani - husababisha tishio kubwa na hatari ambayo haiwezi kufikirika.

**c. Hatua zinazochukuliwa na Benki Kuu**

Baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Benki Kuu kuhusu swala la Cryptocurrency ni pamoja na:

- i. Kuchukua hatua za tahadhari na kutaarifu umma juu ya hatari zilizopo kwa kushiriki katika masuala yanayohusiana na cryptocurrency kwa kutumia vyombo mbalimbali;
- ii. Kuendelea kutafiti na kujifunza teknolojia hii kwa kina kwa lengo la kutafuta suluhisho la kudumu ambalo limezingatia mahitaji ya udhibiti wa masuala ya fedha ya nchi; na
- iii. Kujenga uwezo wa wafanyakazi wanaohusika na usimamizi wa maswala yanayohusu huduma za kifedha zinazotumia teknolojia (ikiwamo cryptocurrency) ili kuweza kusimamia udhibiti ipasavyo.

**42. Zamani kulikuwa na chenji za kutosha mitaani ukinunua kitu unapewa chenji yako, Je kwanini sasa hivi chenji ni shida kupatikana?**

Benki Kuu ina matawi 6 katika kanda 6 ambayo ni Arusha, Mbeya Mwanza, Dodoma, Mtwara na Zanzibar, na inaendelea kufungua vituo mbalimbali vya huduma zake za usambazaji wa fedha katika baadhi ya mikoa kupitia mabenki ya biashara. Kwa sasa vituo hivi ni Bukoba, Kigoma, Sumbawanga, Songea, Pemba, Shinyanga, Tanga na Tabora.

Dhumuni la kusogeza huduma hizi ni kuwezesha kuwafikia wananchi kwa urahisi na haraka. Wananchi wanatakiwa waende kwenye matawi ya Benki Kuu na benki zote za biashara zilizopo karibu na maeneo yao kupata huduma zikiwepo huduma za chenji. Hivyo wananchi wanashauriwa waende kwenye mabenki kupata huduma za chenji na pia ubadilishaji wa noti chakavu.

Benki Kuu inapenda kutoa taaarifa kuwa kupitia matawi yake na mabenki ya biashara chenji za kutosha zinapatikana kuanzia senti 5 hadi shilingi 10,000 kulingana na mahitaji ya wananchi. Noti na sarafu hizo pia zinapatikana katika maeneo yaliyoainishwa hapo juu, isipokuwa hivi sasa inaonekana matumizi ya senti 5 hadi shilingi 20 yamepungua sana hivyo ni wachache tu wanaokuja kuleta mahitaji yao.



**43. Kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko kuwa wafanyabiashara na wenye maduka huko vijijini hukataa kupokea sarafu zinazoonekana zimechakaa toka kwa wananchi; ambao wengi wao hawana uwezo wa kuzipeleka mahali popote, Je ni hatua gani zinachukuliwa kuweza kutoa sarafu bora?**

Noti huingizwa katika mzunguko kupitia katika benki za biashara na kuingia katika mikono mbalimbali ya wananchi na baadae kuchakaa kutokana na mazingira yanayoizunguka. Hali hii ikifikiwa, inatakiwa noti irudishwe kwenye benki eyote ya biashara. Benki za biashara zina jukumu la kurudisha Benki Kuu noti zote chakavu ilizopokea toka kwa wananchi ili kubadilishwa kabla ya kuharibiwa na Benki Kuu. Nia na malengo ya Benki Kuu ni kuhakikisha noti na sarafu safi pekee ndizo zinazotumika kwenye mzunguko wa fedha.

Uchakavu wa noti huletwa na sababu kuu mbili:

- i. Utunzaji usiofaa kwa baadhi ya watumiaji ambao huzitunza katika mazingira yasiyofaa na wakati mwingine kuzishika na uchafu au unyevu wakati wa kununua vitu katika masoko mbalimbali kama vile ya vyakula, mkaa, n.k.
- ii. Kuendelea kuzitumia noti ambazo zinaonekana wazi kuwa muda wake wa kukaa katika mzunguko umefikia mwisho badala ya kuzipeleka benki ili zibadilishwe na noti mpya.

Noti chafu na chakavu ambazo huonekana hazifai kurudi katika mzunguko huondolewa katika mzunguko na kuharibiwa. Benki kuu ya Tanzania inaendelea kuwahimiza wananchi kuhusu utunzaji mzuri wa fedha ili kupunguza uharibifu na uchakavu wa haraka wa noti na sarafu.

#### **44. Kuondolewa kwa noti ya 500/= kwenye mzunguko unasaidiaje wananchi?**

Kuondolewa kwa noti ya 500 kwenye mzunguko kuna faida kubwa kwa wananchi kwa sababu; Noti ya 500 ilionekana kuchakaa haraka, kutokana na kuwa na mzunguko mkubwa ikilinganishwa na noti nyingine na haipitii ule mfumo wa kawaida wa kibenki kurudi Benki Kuu kwa ajili ya kuibadilishwa. Tofauti na matarajio, wananchi wengi wanapopeleka fedha zao benki noti za 500 si miongoni mwa hizo pesa. Wananchi wengi wamekuwa wakipeleka Benki noti zenye thamani ya zaidi ya mia tano kama shilingi elfu mbili, elfu 5 na elfu 10 lakini shilingi 500 au chini ya hapo wamekuwa wanabakiza majumbani kwa ajili ya matumizi madogomadogo. Matokeo yake noti ya shilingi 500 ilikuwa ipo zaidi kwenye mikono ya watu na nadra kurudi kwenye mfumo wa kibenki kubadilishwa ndio maana Benki Kuu ikaona ni busara kuiondoa na kuleta sarafu badala yake.

Kiuchumi hili halina athari yoyote kwani haibadili ujazi wa fedha na kuathiri mfumuko wa bei bali kilichofanyika ni kuondoa noti ya 500 yenye thamani ya 500 na kuleta sarafu yenye thamani ileile ya shilingi 500.